TANGAZO LA SERIKALI Na 1012 la tarehe 6/12/2024.

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

SURA YA 287

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali kuhusiana na madini ya ujenzi;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa au afisa aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mchimba madini" maana yake ni mtu mwenye leseni ya kuchimba madini ya ujenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazotolewa katika eneo la Halmashauri; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyoingia mkataba kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Maombi ya kibali

**4.**-(1) Mtu anayekusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi maombi ya kibali cha kuchimba madini ya ujenzi kwa mandishi kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya kibali yataambatishwa na taarifa zifuatazo:

(a) leseni ya uchimbaji wa madini iliyotolewa na mamlaka husika;
(b) aina ya madini yanayokusudiwa kuchimbwa;
(c) mkataba au uthibitisho wa umiliki pamoja na ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi;
(d) mpango wa utunzaji wa mazingira katika eneo la machimbo; na
(e) muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kijiji ambacho uchimbaji wa madini ya ujenzi utafanyika ukionesha kukubaliana na uchimbaji huo.

(3) Baada ya kupokea maombi na kabla ya kutoa kibali, Mkurugenzi ndani ya muda wa siku saba atakagua eneo ambalo uchimbaji wa madini ya ujenzi unakusudiwa kufanyika ili kujiridhisha iwapo eneo hilo linafaa kwa shughuli za uchimbaji.

(4) Endapo Mkurugenzi ataridhika kwamba eneo linaloombewa kibali linafaa kwa shughuli za uchimbaji atatoa kibali, na iwapo ataona kuwa eneo hilo halifai kwa shughuli za uchimbaji wa madini atakataa kutoa kibali na ataeleza sababu za kukataa maombi.

Wajibu wa mwenye kibali

**5.** Mtu atakayepewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi atakuwa na wajibu wa-

(a) kulipa ada ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kila mwaka;

(b) kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii na masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi;

(c) kuchimba madini ya ujenzi pasipo kuharibu kingo za korongo kwa namna itakayosababisha mmomonyoko au athari kwa mazingira; na

(d) kulipa ushuru na tozo mbalimbali zinazotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii au sheria ndogo nyingine zilizotengenezwa na Halmashauri.

Muda wa uchimbaji na masharti ya usafirishaji

**6.**-(1) Shughuli za uchimbaji na usafirishaji wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri zitafanyika kulingana na muda uliobainishwa kwenye kibali.

(2) Mkurugenzi anaweza kutoa kibali kuruhusu shughuli za uchimbaji na usafirishaji wa madini ya ujenzi kufanyika nje ya muda uliotolewa kwenye kibali.

(3) Kila mmiliki au dereva wa chombo kinachotumika kusafirisha madini ya ujenzi atatakiwa kuhakikisha kuwa chombo hicho kimefunikwa wakati wote wa usafirishaji wa madini ya ujenzi.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

**7**. Afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote yanapochimbwa madini ya ujenzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi na kutoa ushauri wa uendeshaji wa shughuli za uchimbaji.

Ushuru wa madini ya ujenzi

**8**.-(1) Kutakuwa na ushuru wa madini ya ujenzi ambao utalipwa na mchimbaji au msafirishaji wa madini ya ujenzi kama utakavyoainishwa na Halmashauri.

(2) Mchimbaji au msafirishaji wa madini ya ujenzi atatakiwa kulipia ushuru wa madini ya ujenzi kwa viwango vilivyoainishwa katika sheria ndogo ya ada na ushuru iliyotengenezwa na Halmashauri.

(3) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa katika eneo la machimbo, barabara zinazoelekea au kutoka

maeneo ya machimbo au eneo lolote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri.

(4) Mchimbaji au msafirishaji atakayeshindwa kulipa ushuru anaotakiwa kulipa atatakiwa kupakua madini ya ujenzi kutoka katika chombo au kutochukua madini hayo mpaka hapo atakapolipa ushuru anaodaiwa.

(5) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumzuia mchimbaji au msafirishaji kusafirisha madini ya ujenzi iwapo ikibainika kuna ukwepaji wa kulipa ushuru.

Vituo vya ukaguzi

**9**.(1) Kutakuwa na vituo vya ukaguzi wa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi katika njia zinazoingia au kutoka katika maeneo ya machimbo.

(2) Kila dereva wa chombo cha usafiri kilichobeba madini ya ujenzi atatakiwa kusimama katika kituo cha ukaguzi na kuonesha stakabadhi ya kielektroniki inayothibitisha malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi yaliyo katika chombo cha usafiri.

(3) Endapo dereva wa chombo cha usafiri kilikachokamatwa kwenye eneo la machimbo au wakati wa kusafirisha madini ya ujenzi atatoroka, afisa mwidhiniwa au wakala atazuia chombo hicho hadi faini na ushuru unaodaiwa utakapolipwa.

Kufutwa au kusimamishwa kwa kibali

**10.**(1) Halmashauri inaweza kufuta au kusimamisha kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi iwapo itajiridhisha kuwa kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii au masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(2) Kabla ya kufuta au kusimamisha kibali, Halmashauri itatakiwa kutoa notisi ya siku saba ya kusudio la kufuta au kusimamisha kibali kwa mmiliki wa kibali.

(3) Notisi itakayotolewa itaainisha sababu za kufuta au kusimamisha kibali husika.

(4) Endapo kibali kitafutwa au kusimamishwa, mchimbaji atasitisha shughuli za kuchimba madini.

Uteuzi wa wakala

11**.** (1) Halmashauri inaweza kuteua wakala kwa ajili ya kutekeleza majukumu chini ya Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri; na

(c) kutekeleza jukumu lingine lolote kadri atakavyoelekezwa na Halmashauri.

Hasara wakati wa ukaguzi au ukusanyaji wa ushuru

**12.** Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote atakayopata mchimbaji au msafirishaji wa madini ya ujenzi wakati wa ukaguzi au ukusanyaji wa ushuru isipokuwa kama hasara hiyo itasababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Makosa

**13**. Mtu ambaye-
(a) ataanzisha machimbo au kuchimba madini ya ujenzi bila kibali;
(b) atasafirisha madini ya ujenzi bila kulipa ushuru;
(c) atachimba madini ya ujenzi nje ya muda ulioainishwa kwenye kibali;
(d) atasafirisha madini ya ujenzi katika chombo ambacho hakijafunikwa;
(e) atamshawishi mtu au kundi la watu kutolipa ushuru;
(f) atakataa kutii agizo atakalopewa na afisa mwidhiniwa wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;
(g) atamzuia afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza wajibu wake;
(h) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;

(i) atachimba madini katika maeneo yasiyoidhinishwa;au
(j) atachimba madini ya ujenzi kwa namna inayoharibu kingo za korongo.

anatenda kosa.

Adhabu

**10**. Mtu akipatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

**11**. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ada au ushuru wa madini ya ujenzi unaodaiwa.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

### KIBALI CHA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

Kibali hiki kimetolewa kwa Bw/Bi: …………………………………………..……wa S.L.P……………….,.....……….
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa Ameridhia Ndugu mtajwa hapo juu, aendeshe shughuli za kuchimba madini ya ujenzi katika eneo la ……………………..……Kijiji cha………………………. kata ya …………………………… baada ya kufanya ukaguzi katika eneo husika ili kutathimini athari za mazingira.

Kutokana na uzingatiaji wa athari za mazingira mchimbaji anaruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi katika eneo hilo kwa muda wa miezi kumi na mbili tu. Mwombaji analazimika kuomba tena kibali baada ya muda huo kuisha na ukaguzi utafanyika tena.

TAMKO LA MWOMBAJI:
MIMI………………………nipo tayari kufuata masharti ya kibali hiki cha Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya………. kwa lengo la kutunza na kuhifadhi mazingira. Nathibitisha kwa hiari yangu nimeelewa vema masharti ya kibali hiki.

Jina: ………… Saini ………………….. Tarehe …………………

*KWA MATUMIZI YA OFISI TU:*

Mwombaji amelipia Shilingi ……… tarehe……….mwezi…….Mwaka…………

(Ambatanisha stakabadhi ya malipo na fomu hii)

Jina la Afisa aliyetoa kibali………… Saini …………… Tarehe ……………
Muhuri: …………………………………

---

JEDWALI LA PILI

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 11)*

FOMU YA KUKIRI KOSA

Mimi…………………………………………………….…NAKIRI KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya .…… ya Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka, 2024

NAKUBALI kulipa kiasi cha shilingi.......... cha ada au ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ya shilingi.........

NATHIBITISHA KWAMBA, maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa MIMI MWENYEWE na kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo hii tarehe………….ya mwezi…………..… mwaka 20…………….
Jina……………………………….....
Saini………........…………………......

MBELE YA MKURUGENZI

Jina:…………………......................................
Saini:…………………..…..............................
Tarehe:..............................................................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 9/11/2023 mbele ya-

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa*

MWENYEKITI,
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
29 Oktoba, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (Mb.),
*Waziri wa Nchi- OR-TAMISEMI*,